


COMPANY HIGHLIGHT

# Mfuko wa Jamii

na Kennedy Haule

## Utangulizi

Tangu KVTC ilipoanzishwa 1992, iliunda mfuko wa jamii kusaidia jamii ya vijiji waliokuwa na mazoea ya kutumia ardhi ya KVTC kabla kumilkishwa na kampuni.

Mfuko wa jamii uliundwa kuboresha miundo mbinu ya jamii inayo tuzunguka na inajikita zaidi kwenye maswala ya elimu, afya na kuboresha miundo mbinu ya kiuchumi. Mfuko haufadhili shughuli za kisiasa au za kidini.

Kuanzia 1992 – 2000 Mfuko wa jamii ulipitishia fedha kwa asasi isiyo ya kiserikali (NGO) na halmashauri ya wilaya hata hivyo kuanzia 2000 hela zililipwa moja kwa moja kijijini.

## Eneo linalohusika

Tangu uanzishwe Mfuko wa Jamii umepanuka kutoka vijiji 9 mpaka 17 kutokana na kushirikisha vijiji jirani na kugawanywa vijiji kutokana na idadi ya watu. 2009 kijiji cha Mavimba kiliongezwa kutokana na kujengwa kiwanda na kuhamishiwa kwa makao makuu.

## Uchambuzi wa Mradi

Halmashauri ya kijiji itatambua mradi wa jamii na kuwakilisha kwa uongozi wa kampuni kwa uchambuzi wa awali. Kama mradi umetimiza vigezo vya mfuko wa jamii, hatimaye halmashauri ya kijiji inawakilisha mradi kwenye mkutano wa wananchi wote kwa kupigiwa kura na kusaini. Wakifanikiwa kuwakilishi, kampuni inaruhusu fedha kuchukuliwa na inafuatilia utekelezaji. Halmashauri ya wilaya na vilevile Mkuu wa Wilaya wana arifiwa juu ya mradi wowote ulioidhinishwa na vile vile wakati wa kumaliza.

## Miradi Iliyofadhiliwa na Athari

Kuanzia 2000 wakati msaada ulipokuwa unapitishiwa moja kwa moja kupitia akaunti za kijiji kuna fedha shilling milioni 700 zilitolewa kusaidia jumla ya miradi 140 mingi yao ikihusiana na elimu na kusoma.

Mara nyingi hela ya mfuko wa jamii ina tumika na fedha nyingine kutekeleza mradi na kwa hiyo athari kwa jumla na thamani ya miradi kubwa kuliko ilivyo ripoti wa hapa juu.

## Kwa taarifa zaidi

Meneja Jamii KVTC anaweza kupa taarifa za nyongeza juu ya Mfuko wa Jamii. Unaweza kuwasiliana naye kwa simu namba **0757 768 825** au khaule@kvtc-tz.com

HIGHLIGHTS



## Uhifadhi wa wanyama!

Jirani na kiwanda chetu tunatunza karibu hekta 60 ya misitu mizuri ya miombo na licha ya kelele za machine wanyama wanaingia.

Kwa sasa tuna bushbuck, duiker na chui akiwa na watoto wanazunguka kwenye msitu karibu na kiwanda.

## African Forestry

KVTC ni mwanachama African Forestry (AF), shirika linalowakilisha viwanda na biashara sekta ya misitu, Kujua zaidi wasiliana kupitia barua pepe info@africanforestry.org au tovuti yao www.africanforestry.org

# Kutoka Dawati la Hans

na Hans Lemm

Kheri ya mwaka mpya na karibu kwa makala ya kwanza ya kijarida cha KVTC kinachotolewa kila baada ya miezi mitatu. Ingawa mwaka ndio tu umeanza kwa wafanyakazi wa KVTC ilikuwa imesha anza kwa kipindi hivi tulianza shughuli zetu Disemba.

Huu mwaka tumebarikiwa kupata mvua mapema iliyo anza tayari Oktoba na imeendelea mpaka mwisho wa mwezi January na sasa tuko katika ya kipiindi cha ukame, kawaida tunakiona kabla ya kipindi cha mvua za mda mrefu March na April.

Shughuli za upandaji ziko katika kiwango cha juu mashambani kwetu na vilevile kwa mashamba ya wakulima yatapandwa hivi karibuni. Jumla ya hekta 250 zitapandwa kwa wakulima wa nje mwaka huu.

Mwishoni mwa Disemba tulikuwa na mabadiliko katika wafanyakazi baadhi ya mameneja walienda kwenye shughuli nyingine au waliamua kuwa karibu na familia zao. Kwa bahati tuliweza kuvutia kijana na mwenye kipaji mfanyakazi mpya atayeleta mawazo mapya KVTC.

Tume hamasika na changamoto ya uzito uhai ulio anzishwa mwaka jana na tunamatumaini kupata mapendekezo makini na yanayo fanyakazi na tumaini jitihada zitaleta matokeo na kwa nyongeza kuimarisha uchumi wa kiwanda hapa (na kitaifa).





*Kampuni ya KVTC ilishiriki katika mazungumzo ya kuandaa sera mpya ya misitu yaliyofanyika Morogoro tarehe 18/01/2018.*

# The KVTC Biomass Challenge

na Hanta Rwegoshora

Tarehe 14/12/2017 Kampuni ya KVTC ikishirikiana na Shirika la Private Forestry Programme (PFP) ilizindua mpango mkakati wa kukabiliana na taka ambazo ni mabaki yatokanayo na uvunaji na uchakataji wa mazao ya misitu kwa kutumia mabaki hayo kuzalisha nishati mbadala.

## Sherehe ya uzinduzi

Mnamo tarehe 14/12/2017 Kampuni iliwaalika washirika wake wa karibu kwenye tafrija fupi ambayo ilifanyika kwenye Hoteli ya Coral Beach Dar es Salaam.

Tafrija hii ilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Muungano Mhe. January Makamba akiwa mgeni rasmi na alifuatana na Balozi wa Finland ambao kwa pamoja walizindua mpango mkakati wa kukabiliana na taka zitokanazo na mazao ya misitu.

## Historia

Wananchi walio wengi nchini Tanzania wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya nishati na ongezeko la watu kwa sasa linazidisha msukumo mkubwa kwenye ukataji wa miti na hivyo kuhatarisha uwepo wa misitu endelevu.

KVTC inamiliki na kuendeleza mashamba ya misitu pamoja na kiwanda cha mbao katika wilaya ya Ulanga mkoa wa Morogoro. Pia kampuni inauza baadhi ya magogo kutoka kwenye mashamba yake kwa viwanda vingine vinne ambavyo viko maeneo ya jirani. Viwanda vyote hivi vinazalisha kwa kiwango kikubwa taka zitokanazo na uchakataji wa mazao ya misitu.

KVTC inaamini mabaki ya mazao ya miti yatokanayo na uchakataji yanaweza kuwa suluhisho la kudumu kwa mahitaji ya nishati kwa kuwa mbadala wa kuni na mkaa na hivyo kusaidia kupunguza uharibifu wa misitu, wakati huo huo ikitoa fursa za kiuchumi kwa kampuni kwa kuongeza mapato yatokanayo na mabaki ya misitu.

## Zawadi

KVTC inawaalika wadau ambao wangependa kuwasilisha Mpango wa Biashara kwa ajili ya kukabiliana na taka zitokanazo na uvunaji na uchakataji wa mazao ya misitu. Uongozi wa Kampuni pamoja na ule wa Shirika la PFP umeandaa Majaji ambao watapitia kwa umakini wa hali ya juu na kuamua Mpango wa Biashara bora na mshindi atazawadiwa fedha taslimu **Tshs 75 milioni**

Ili kupata maelezo kamili namna ya kushiriki tafadhali tembelea tovuti yetu: http://kvtc-tz.com/the-kvtc-biomass-challenge/

### 20-21 MARCH: FORESTRY TRADE FAIR

Tarehe 20 mpaka 21 Marchi 2018 Private Forest Programme (PFP) imeandaa maonyesho ya biashara ya misitu Mafinga. KVTC itaonyesha bidhaa zake. Maelezo Zaidi tembelea tovuti ya PFP: http://www.privateforestry.or.tz

### TUSIKILIZE

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

### JE UNAJUA?

Mti mkubwa kabisa wa mtiki duniani unapatikana Myanmar na kipenyo cha mita 8.4 na urefu wa mita 33

### WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE:
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ